...Mwandishi wa vitabu, Zabacha Deus akiwa kwenye picha ya pamoja na wanafunzi wa shule za Feza, baada ya kuwakabidhi vyeti vya uandishi bora wa vitabu nchini katika hafla iliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. (Na Mpiga Picha Maalumu).

## MTAZAMO

RAIA MWEMA UK 7

# Kupanda bei ya nyama kutufikirishe

**Na Joseph Kulangwa**

**NYAMA** ni chakula muhimu katika jamii yoyote ile duniani. Ndiyo sababu huchukuliwa kama chakula cha heshima, kutokana na kwamba katika karibu kila hafla au shajara nyama haikosekani.

Kwa miaka nenda rudi, nyama imekuwa kichocheo muhimu katika kuheshimisha wageni wafikapo ugenini, ambako watachinjiwa mnyama au hata ndege ilimradi nyama inakuwa ni sehemu ya chakula.

Mijini ukisikia mishikaki ujue ilianzia kwenye nyama, ingawa siku za karibuni kumekuwa na mishikaki ya samaki hata ya matunda, halikadhalika nyamachoma imekuwa maarufu mijini na hasa katika sehemu nyingi za starehe.

Katika familia nyingi, itokeapo sikukuu, nyama huwa ndicho chakula kikuu cha siku hiyo, ambapo mboga za majani husahaulika, licha ya wataalamu kushauri watu kula mboga kuliko nyama, kutokana na sababu za kiafya.

Lakini pamoja na yote hayo, bado nyama inaendelea kushika usukani katika vyakula vyenye heshima katika jamii. Ndiyo sababu nyama ikosekanapo siku muhimu za sherehe huwa ni kizaazaa na watu kutafutana.

Mara nyingi hususan katika siku kuu za Kiislamu, nyama hupewa kipaumbele, ambapo baada ya Hija mathalan, Mwislamu huchinja na kutoa nyama kama sadaka kwa wasiojiweza. Hivyo heshima ya nyama huendelea kudumishwa.

Nyama ikipanda bei huwa ni matatizo na malalamiko kutoka kwa walaji, ambao hujikamua angalau mara moja au mbili kwa wiki kupata kitoweo hicho.

Wafugaji hupewa heshima kutokana na kufuga wanyama ambao ndio huzalisha nyama. Hupandisha bei ya mifugo yao kutokana na sababu mbalimbali, hivyo wasio na mifugo kuumia kwa kujikamua zaidi ili kupata kitoweo hicho.

Nchini hivi sasa, hususan katika Jiji la Dar es Salaam, bei ya nyama imepanda. Malalamiko yako kila kona. Bei ya sasa ni kati ya Sh 8,000 na Sh 10,000 kwa kilo moja ya chakula hicho.

Hali hiyo imesababisha kelele nyingi na kilio hapa na pale hata wananchi kuitaka Serikali iingilie kati na kuweka bei elekezi kama inavyofanya kwa baadhi ya bidhaa kama vile mafuta jamiii ya petroli.

Serikali nayo kupitia Bodi ya Taifa ya Nyama, inasema sababu kuu ni maendeleo ya kiuchumi; kwamba hivi sasa nchi ina viwanda 35 vya kuchakata na kusindika nyama kwa ajili ya kuuza kwa walaji.

Lakini katika viwanda hivyo, vitano vinasindika nyama na kuiuza Ughaibuni sehemu za Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali, hivyo nyama kuhitajika kwa wingi kwa ajili ya kulisha viwanda hivyo.

Matokeo yake ni kupungua kwa wachinjaji wadogo, hivyo nyama kuadimika na kulazimika kuuzwa kwa bei hiyo ya kuruka na kuishia walaji wa nyama kukosa mbadala na kubaki kugugumia kwa maumivu.

Yapo mapendekezo ambayo nami nayaunga mkono, kwamba ifike mahali Serikali iingilie kati hususan katika utaratibu wa ununuzi wa nyama, na kuondokana na utaratibu wa mnunuzi au mteja kulazimika kununua kwa kilo.

Hivi sasa mteja ananunua nyama kwa kipimo cha robo kilo, nusu kilo, robotatu ya kilo au kilo moja na kuendelea. Hali hiyo inafanya mnunuzi kukosa chaguo na hivyo kulazimika kununua kiwango kinachopangwa na mwenye duka la nyama.

Kwa nini sasa nyama isianze kuuzwa kwa kiasi cha pesa alichonacho mtu, badala ya kilo, kwa maana kwamba badala ya mtu kufika buchani na kutaka apimiwe nyama kwa uzito, auziwe nyama kulingana na pesa aliyonayo.

Mathalan aweze kununua nyama kwa Sh 2,000 au hata Sh 1,000 kulingana na pesa yake badala ya kutumia vipimo vya uzito, ambavyo mara nyingi hulazimisha kipimo cha chini kuwa robo na kilo moja na kuendelea.

Ufike wakati mtu akifika buchani atake nyama ya bei fulani na si ya kilo fulani, ili kuondokana na kilio cha kilo ya nyama ya Sh 10,000. Ikishindikana hiyo, basi Bodi ya Nyama iangalie jinsi ya kuhakikisha nyama za wanyama wengine zinaliwa ili mradi zisiwe na madhara.

Tunaweza kuwa kama ndugu zetu wa Mashariki ya Mbali ambao hakuna kiumbe chenye miguu minne kisicholiwa nyama. Mpo hapo?

Scanned with CamScanner